



Zaburi 65:4-13

[4]Heri mtu yule umchaguaye,  
Na kumkaribisha akae nyuani mwako.  
Na tushibe wema wa nyumba yako,  
Patakatifu pa hekalu lako.

[5]Kwa mambo ya kutisha utatujibu,  
Katika haki, Ee Mungu wa wokovu wetu.  
Wewe uliye tumaini la miisho yote ya dunia,  
Na la bahari iliyo mbali sana,

[6]Milima waiweka imara kwa nguvu zako,  
Huku ukijifunga uweza kama mshipi.

[7]Wautuliza uvumi wa bahari,  
Uvumi wa mawimbi yake,  
Na ghasia ya mataifa;

[8]Kwa hiyo wakaao mbali kabisa huogopa ishara zako; Milango ya asubuhi na jioni  
waifurahisha.

[9]Umejilia nchi na kuisitawisha,  
Umeitajirisha sana;  
Mto wa Mungu umejaa maji;  
Wawaruzuku watu nafaka  
Maana ndiwe uitengenezaye ardhi.

[10]Matuta yake wayajaza maji;  
Wapasawazisha palipoinuka,  
Wailainisha nchi kwa manyunyu;



*Waibariki mimea yake.*

*[11]Umeuvika mwaka taji ya wema wako;  
Mapito yako yadondoza unono.*

*[12]Huyadondokea malisho ya nyikani,  
Na vilima vyajifunga furaha.*

*[13]Na malisho yamevikwa kondoo,  
Na mabonde yamepambwa nafaka,  
Yanashangilia, naam, yanaimba.*